

USHIRIKA

 ...katika koo langu kutokana na ibada kadha, ibada kumi na tano huko Arizona. Tulikuwa na wakati mzuri sana. Bwana Yesu alitubariki mno. Walijaribu kufanya maarifa madogo ya vita vya Bwana, natumaini hivi, ndivyo ingekuwa sahihi kufanya. Kupenyeza ndani na kupafyatulia risasi mzunguko mahali pale, kwanza. Niliingia mle siku nyingi kabla ya wakati, nikafanya ibada kumi au kumi na mbili katika makanisa yote makubwa kote Phoenix, Sunnyslope na Tempe na Mesa na chini kote kule, na kupafyatulia risasi mzunguko kwa namna fulani mahali hapo pote kisha kupaongoza pote kwenye mkutano wa siku tano usiku. Na ulikuwa mkutano mkubwa kuliko mikutano yote tuliyowahi kuwa nayo katika Marekani ya Kaskazini. Ulikuwa mkubwa sana. Kiamshakinywa kikubwa kuliko vyote, na—na pia karamu usiku ule.

² Nisingeweza kusema ni wangapi ambao walimpokea Roho Mtakatifu. Lilikuwa—lilikuwa jambo kuu sana jinsi wengi walivyompokea Roho Mtakatifu, na ni wangapi waliponywa na kuokolewa, ni—ni la kustaajabisha zuri mno. Kwa hiyo tunamshukuru Mungu tuyaonapo majira yanasonga mbele. Watu wengi maarufu walikuja. Mmoja wa . . .

³ Hili litamfaa sana Ndugu Neville. Nilimwona mchungaji wa Kipresbiteri, kutoka Chuo cha Kipresbiteri maarufu kuliko vyote katika—katika taifa, akicheza katika Roho. Loo, jamani, lilikuwa jambo la ajabu kweli, alipokea Roho Mtakatifu. Na halafu aliniambia, akasema, “Nina mojawapo ya kanda zako.” Kasema, “Haikuwa nzuri sana.” Kasema, “Haikuwa laini, lakini,” kasema, “niliichukua moja kwa moja mpaka chuoni mwangu na kuicheza.” Akasema . . . Akiwa ndiye mtu maarufu wa saikolojia kule, aliwanyamazisha wote. “Vema, basi walipata kuisikiza mara moja, haidhuru,” akasema. Kisha akasema ali . . .

⁴ Basi akasema akawa anacheza katika roho kanisani mwake, baada ya kumpokea Roho Mtakatifu, nao wakasema, “Kasisi, utajifunza lini mtindo mpya?”

⁵ Akasema, “Wakati kusanyiko langu watakapojifunza huu.” Nikawaza hilo lilikuwa zuri sana, unajua, ukasisi wa Kipresbiteri, ndiyo, kasema, “Wakati kusanyiko langu watakapojifunza mtindo huu.” Kwa hiyo hilo ni jambo zuri. Kama tu mtoto mchanga, akiwa ndio azaliwe na hata hivyo amekuwa . . . Vema, unajua nini ingempasa kuwa, kuwa profesa wa saikolojia katika Chuo cha Kipresbiteri maarufu zaidi ya vyote katika Boston, vema, kiko katika Marekani.

⁶ Nimemwona mmoja wa madaktari maarufu sana wa kupasua moyo wa Mayo akihubiri Injili katika Roho na kunena kwa lugha. Loo, jamani! Nimemwona mtaalamu mwingine, ambaye alikuwa Seventh-day Adventist, kutoka . . . Alikuwa m—m—mtaalamu wa moyo na koo pia, na yeye, mwanamume mzee, alipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Aliupokea. Usiku mmoja nilimwekea mikono huko uwani, naye akampokea Roho Mtakatifu. Kwa hiyo tuna . . . mambo mengi sana ambayo Bwana wetu alitenda ambayo tunashukuru kwayo, na hasa kuyaona wakati huu.

⁷ Halafu nikawaambia, “Mnatambua huu ni wakati gani wakati mwanamwali mpumbavu anapoanza kuomba mafuta?” Hapo ndipo Bwana Arusi alipokuja, nao hao watu, waliokuwa tayari wakaingia. Lo, ninafurahi sana kujua kwamba tunaishi hapa katika siku hizi za mwisho. Unaona? Ninaamini kwamba tunaishi katika moja ya nyakati kuu sana ulimwengu umewahi kujua, karibu kabisa na kuja Kwa Bwana. Je, hilo si zuri sana? Fikiria, kwamba karibu wakati wo wote sasa, Maandiko yote karibu yametimia! Na kwa hiyo tunamtarajia Yeye wakati wo wote. Nasi tunapaswa kuishi chini ya matazamia ya namna hiyo, kwamba, mnamo wakati wo wote linaweza kutukia. Ombeni sana, jitayarisheni!

⁸ Kwenye baadhi ya mazungumzo ya mahojiano leo, mimi, mmoja, nilikutana na mmishenari kutoka Formosa, mwanamke shujaa, mwenye umri wa miaka sabini na mitatu, naye angeonekana kama mwenye umri wa miaka arobaini na mitano. Naye bado ni—ni Binti, na lazima alikuwa msichana mrembo sana. Naye alisema alikuwa amelelewa katika nyumba ya Kikristo ambamo “ndiyo” ilimaanisha ndiyo, na “la” ilimaanisha la. Naye amekulia katika mafundisho hayo makali. Basi akasema, “Ndugu Branham, kwenye umri wa kama, ah,” kasema, “kama umri wa miaka minane, nilifikiri kwamba niliyatoa maisha yangu kwa Bwana Yesu.” Akasema, “Kwenye umri wa kama miaka ishirini, nilishawishiwa na mhudumu fulani wa kimadhehebu, kwamba yanibidi nipate baraka ya hatua ya pili,” akasema, “basi nikadanganyika vibaya sana katika jambo hilo.” Lakini akasema, “Yapata umri wa miaka kumi na saba, nilimpokea Roho Mtakatifu kweli.” Na yeye amerudi hapa sasa akijaribu kuyaamsha baadhi ya haya makanisa ya Kibatisti yanayolala. Alisema kwamba kama—kama kulikuwa na cho chote ambacho ameona “kimekufa,” yeye mwenyewe ni Mbatisti, alisema, “ni haya makanisa ya Kibatisti yaliyokufa nyuma huku,” Aliyaita “vyumba vya maiti.”

⁹ Nikasema, “Vema, nadhani unapokuwa katika mstari wa mbele wa vita . . .” Nafikiri sasa yeye ni . . . Hebu fikiria, mimi, hamsini na miwili, alikuwa kule nje kama mmishenari kabla ya mimi kuzaliwa. Na basi nafikiri nilikuwa ninazeeka sana kuendelea na kazi. Nami nikafikiri, “Lo, nisamehe, Bwana.”

¹⁰ Naye mwanamke huyo, mzima, akiwa mchangamfu na mwenye busara kama tu angeliweza kuwa. Na halafu akinisimulia matukio mbalimbali njiani, na jinsi ambavyo injili ilihitajiwa huko Formosa na—na China, na Japan, na kadhalika. Kwa hiyo walimrudisha kutoka kazini, kasema, “Huwezi kuingia kazini wakati umepita sabini.” Kwa hiyo wakamrudisha. Lakini hatatulia, anakwenda kwenye mikutano hii yote ya Kibatisti. Naye akasema, “Billy Graham,” alisema, “jinsi yeye alivyokuwa anauchukua ujumbe wa Kibatisti, alikuwa anawajibika kwa kanisa la Kibatisti.” Kasema, “Hawachukui mbali vya kutosha kupata Roho Mtakatifu,” alisema. Loo, dada, wewe dumu kabisa na hilo. Hilo ni sawa. Akasema, wale Wachina nyuma kule, kasema asingewaachilia waendeleo mbele na kusema, “Tunamwamini Yesu Kristo.” Kasema, “Hilo lilikuwa sawa,” lakini aliwafanya wakae pale mpaka kitu fulani kitokee, na ndipo wakawa Wakristo halisi.

¹¹ Nikasema, “Hivyo ndivyo jinsi hilo linavyokwenda, dada. Waambie tu, waache wakae mpaka jambo fulani litokee.”

¹² Vipi kama mitume wangesema, sasa, baada ya siku tisa, “Tunaamini kwamba tumempokea Huyo, unaona, na tuliamini tu kwa imani kisha tuendeleo na kazi yetu.” Unaona, lisingetenda kazi. Walingojea hapo mpaka wakajua kwamba jambo fulani limetukia. Na hiyo ndiyo shida yetu leo, hatukai kirefu vya kutosha. Vema, hiyo ndiyo sababu baadaye tunaweza kuishi maisha ya namna yo yote, kufanya cho chote, haitufadhaishi, kwa sababu hatukai pale kirefu vya kutosha. Leo tuko ndani, kesho tuko nje, na *huku* na *huko*. Kama tukikaa kirefu vya kutosha mpaka uingie ndani ufunge mlango nyuma yako, utadumu mle basi. Umetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wako. Ninafurahia sana jambo hilo.

¹³ Nasi tulikuwa na wakati mzuri sana, kama nilivyosema, huko Phoenix na kupitia kote bondeni na wengi wa Wakristo kule, wengi wao wakidumisha maisha yao ya thamani.

¹⁴ Nilikwenda hadi South Mountain, mke wangu nyuma kule pamoja na mimi, siku moja wakati marafiki... Kaka yangu Doc alikaa na wale wasichana wawili, na—na Ndugu na Dada Wood walikaa na mvulana, na mimi na mke wangu tulikuwa na fungate ya pili. Naye akasema, “Bill, unajuja, hii ilikuwa fungate zuri zaidi kuliko ile ya kwanza.” Akasema, “Mara ya kwanza tulipofanya fungate, kitu pekee nilichofanya ilikuwa kukaa kambini na kukungojea uje kutoka mawindoni,” alisema.

¹⁵ Kwa namna fulani nilitumia mbinu dogo, unajua. Niliwaza, “Vema, sasa, sina hela nyingi. Niliweka tu akiba katika mkebe wa poda, kiasi cha kutosha kwenda mawindoni, na bado nilikuwa nioe mwishoni mwa mwaka ule. Kwa hiyo niliwaza, “Basi nitayafanya yote pamoja,” wajua. Na wakati nilikuwa ninakwenda mawindoni, itakuwa fungate, unajua, na kwa hiyo

tukaviunganisha. Lakini wakati huu tuliingharimia na tukatoka kweli tukaenda, na ku . . . tulikuwa na wakati mzuri sana.

¹⁶ Na wengi wao walikuja kutoka kwenye maskani hapa. Nadhani Ndugu Sothmann, jamaa yake nyuma kule, na Ndugu Tom Simpson na wengineo, na Ndugu Maguire, na sisi sote tulikuwa na wakati mzuri sana katika Bwana.

¹⁷ Na kwa hiyo tukaenda hadi South Mountain, ambako ni Kusini tu mwa Phoenix, na kuondoka kwenye msongo ule. Aha! Msongo katika mji wa kisasa! Si ajabu watu walipoanza kuongezeka juu ya uso wa nchi, dhambi, na ujambazi viliingia. Nami nikatazama juu kule, na huku tukiketi juu sana ili tuweze kuona bonde la Phoenix, nilimwambia mke wangu, “Nashangaa ni mara ngapi, tangu tumeketi hapa katika dakika hizi kumi na tano, Jina la Bwana limetajwa bure katika jiji lile?”

¹⁸ Kama, vema, katika jiji na vitongoji vyake, tukichukua Tempe na—na Sunnyslope na kule kote. Nafikiri kuna yapata watu milioni moja katika bonde lile. Nikasema, “Miaka mia tatu iliyopita hapakuwa na cho chote ila mipungate na mbwa mwitu hapa. Na hilo labda, machoni pa Bwana, lingefaa kama lingelikuwa kama lilivyokuwa.” Hiyo ni kweli. Ingawa lile—lile jiji maarufu ambalo walijenga hapo, na nyumba nzuri na kadhalika, zinapendeza. Lakini ingekuwa sawa, ingefaa zaidi kama wanaume na wanawake walikuwa wakienda huku na huko barabarani wakiinua mikono yao hewani, wakimtukuza Mungu na kumshukuru Yeye. Lakini, badala ya jambo hilo, ni kulaani, kufanya yasiyofaa, kunywa. Hebu achilia tu ustaarabu uingie, nao uovu uko.

¹⁹ Nikasema, “Kuna kuzini kungapi kumetendeka jana jioni, usiku wa jana katika jiji hili! Walevi wangapi! Nyumba ngapi. . . Mangapi—mambo mangapi yasiyofaa yametendwa saa moja iliyopita, katika jiji hili maarufu!”

²⁰ Naye mke wangu akaniambia, alisema basi kitu kama hiki, kama nilivyowaza, “Kungekuwa na faida gani ya kuja hapa basi? Kwa nini umeondoka nyumbani ukaja huku?”

²¹ Ndipo nikasema, “Jambo ni hili. Baada ya hayo yote, ambao hakika ndio wengi, lakini kuna kundi dogo chini kule. Sala ngapi za kweli zilipaa kwenda juu jana jioni chini kule, wakija kwenye ibada?”

²² Na Yeye alikuwa mwema mno kwetu hata makanisa yangejaa kabla ya jua kuchwa, hata usingeliweza kuingia kwenye viwanja karibu na mahali pale. Na hayo madhehebu na kadhalika, na Bwana alimwaga Roho Wake na kuwabariki. Nami sikusitasita, niliendelea tu kutangaza Injili moja kwa moja. Na wakati mwingine, bila shaka ni chungu sana, bali ndiyo njia pekee ninayojua. Ni chungu humu. Hivyo basi itakuwa chungu zaidi hukumuni ambapo itatubidi kuistahimili. Kwa hiyo, kwa jumla, lilikuwa jambo tukufu sana. Na tunataka kulishukuru

kanisa hapa kwa kuomba na kutusaidia, na—na kutusogeza karibu na msalaba.

²³ Na sasa hapo nilipokuwa nikirejea nyumbani, humu, na ningeshuka asubuhi hii pengine kuwaombea baadhi ya wagonjwa. Nina mahojiano mengi ambayo yanangojea, visa, ambavyo baadhi yao nimevipata siku chache zilizopita tangu nimekuwepo hapa, vimengojea mwezi mmoja tangu niondoke. Kwa hiyo wanajaribu kuwaendea upesi wawezavyo, kuwachukua toka sehemu mbalimbali wanakokaa.

²⁴ Na Bwana akipenda, mnamo majuma mawili zaidi, nitakwenda Tucson, hiyo ni kushuka sehemu ya chini. Na sasa wafanya biashara wakati huu, kwa hiyo mnaweza kuliombea jambo hili... Sitaki kamwe kutenda kitu cho chote mpaka kwanza niamini ni mapenzi ya Bwana. Sasa, mkutano unaofuata ni wa huko Modesto halafu toka hapo hadi Washington, jimbo lenyewe, Washington, na hadi Zurich, na halafu Palestina, na halafu tuende Afrika Kusini. Na hayo yote yanafanyika kati ya sasa na Juni. Nami nilialikwa kuwa mzungumzaji kwenye mikutano yote hii. Na huenda likanipa nafasi ya kuingia Afrika Kusini tena. Mwito wao, kila mwezi tunapata makaribisho. Bali kama mmoja...

²⁵ Kuna mtengano mkubwa katika makanisa, makanisa ya Kipentekoste. Na kama ukienda upande mmoja, yale mengine hayatajishughulisha na jambo hilo. Nao hawatashirikiana pamoja, kwa hiyo nimejizuia sasa kwa yapata mika mitano nikiwa na mwito moyoni mwangu wa kwenda. Na sasa, pengine kama wafanya biashara watanikaribisha, kiasi tu cha kupata kujiimarisha, hiyo ni kutoka pande zote mbili, unaona, na kwa hiyo hili huwafanya hao wote kukutanika pamoja. Yawabidi wote washirikiane katika jambo hilo kwa sababu haja zao za kifedha za—haja za makanisa yao zipo, kwa hiyo yawabidi waje kusudi wasione haya, unaona. Kwa hiyo pengine yawezekana iwe ni mapenzi ya Bwana, hata hivyo, sijui. Linaonekana jema, lakini sijui.

²⁶ Ndipo basi, katika mwaka huu, Ndugu Borders alinipa utaratibu wa safari au mialiko. Na, kwa kweli, ilikuwa ni kitabu kikubwa mara mbili namna *hii* cha mialiko kila mahali ambayo imekuja tangu Krismasi iliyopita. Ni kazi kubwa kabisa kwa akili ya binadamu kujaribu kulitatua, kwa hiyo sikuchukua wo wote. Nitachukua mkutano mmoja tu, ndipo ningoje nione ambako Bwana ataniambia niende tokea hapo, ndipo nitakwenda mwingine, na halafu mwingine, na po pote Yeye aniambiapo niende. Kwa hiyo, niombeeni.

²⁷ Nakumbuka mwaka uliopita, kule chini na Ndugu... au kwa Dada Cox chini kule, wakati Ndugu Arganbright aliponiita kufanya safari hii hadi Anchorage. Vipi kama ningeendelea na hiyo kwa kubahatisha tu kwamba yote ni sawa?

²⁸ Sasa, nilikuwa ninafikiria jambo hilo, *kubahatisha*, nilihubiri juu ya somo la jambo hilo. Nilisema nilipokwenda nje kule, niliwaambia vijana wa kanda, “Msichukue kanda zo zote. Msitoke na kanda zo zote, nitahubiri juu ya masomo yale yale niliyohubiri hapa.” Nafikiri nilihubiri moja ambalo nilihubiri hapa, mengine yote yalikuwa mapya. Na Ndugu Maguire aliyanasaa, yote.

²⁹ Kubahatisha. Kwa hiyo kama ningelikwenda, *nikibahatisha* juu kule, hakika ingekuwa tofauti na ilivyotokea kuwa, lile ono lisingelitimizwa. Lakini lile ono lilitimilizwa, na ninyi nyote mnajua jambo hilo, jinsi Bwana alivyobariki.

³⁰ Sasa, kuna jambo jingine ambalo limekuwa moyoni mwangu muda mrefu. Kanisa, liombeeni. Ninyi watu wote hapa mnajua kwamba tangu nilipokuwa mvulana mdogo sikuridhika kamwe katika nchi hii. Moyo wangu wote umetamani sikuzote kwenda Magharibi. Na ninakumbuka nilipokuwa ninamfyekesa majani mama mkwe wangu kule juu kwenye mahali padogo ambapo palikuwa mali ya kanisa hapa, kwamba mahali pale... Nilikuwa nimeketi kwenye vipandio, ndipo Roho Mtakatifu akanizungumzia, akasema, “Siwezi kukubariki zaidi mpaka unitii Mimi kabisa, kama Ibrahimu.” Unaona? Na, Ibrahimu, Mungu alimwambia ajitenge na aende peke yake. Na, alipofanya hivyo, alimchukua baba yake na mpwake. Ndipo Ibrahimu alipomtii Mungu kabisa, basi kulikuwa na utimilifu kabisa wa kile Mungu alichomwahidi. Na kifungo, moja ya vifungo muhimu ambavyo vimenifunga mimi hapa, kilikuwa mama yangu. Mnajua hivyo. Na sasa mama ameondoka kwenda kuwa pamoja na Bwana Yesu. Na si—sijui nigeukie njia gani, nifanyeje, kwa hiyo niombeeni.

³¹ Sasa, Ndugu Neville, nilitoka kwenda jukwaani, niliwaza, “Vema, nitakwenda kule nje.” Mtu fulani alikutana nami akasema, “Loo, wana ibada nyingi kuu usiku wa leo.” Kasema, “Watakuwa na ibada ya mahubiri, ibada ya nyimbo, ibada ya maombi, halafu wachukue sadaka, na halafu wakasema wana—watatawadhana miguu, ushirika, na ibada ya ubatizo.”

³² Nikawaza, “Maskini ndugu yangu! Jamani! Jamani, yote hayo, najua hilo ni nini, labda baada ya kuhubiri sana asubuni ya leo.” Sasa, nikawaza, “Nitaingia juu kule, pengine atanitaka niongoze ushirika.”

³³ Naye akasema, “Utatuzungumzia usiku wa leo kama ukijisikia unaongozwa?” Kwa hiyo ninajua hilo linamaanisha nini. Kwa hiyo basi nikarudi nikachukua Andiko hapa na kuandika maelezo machache, na pengine Bwana atanisaidia kutoa ujumbe mfupi wa kama masaa manne, na halafu tuta—tutatawadhana miguu, halafu ushirika. Na—na, loo, mimi, labda nitamaliza kabla ya hapo. La, nilikuwa ninawatania tu. Kama dakika ishirini, thelathini, na halafu tutakuwa

na ubatizo, kutawadhana . . . Nini kinachofuatia hii, ushirika? Ushirika unafuatia hii, halafu ibada ya ubatizo.

³⁴ Sasa, tunafurahi kwamba mtabatizwa. Sasa, kama Mungu akipenda na hilo likimpendeza Yeye, na ni sawa kwa mchungaji na watu, Jumapili ijayo asubuhi nitashuka kuja kuwaomba wagonjwa, na kuzungumza, Bwana akipenda, Jumapili hii ijayo, sababu labda Jumapili ifuatayo nitakuwa nimeondoka tena wakati huo. Na sasa nikiwa humu, nataka kuja na—na kuzungumza hapa, sababu labda kwa namna fulani tuna uhusiano wa pamoja kama ndugu, na mimi pamoja na Ndugu Neville hapa, na sisi—sisi tunapendana, na tu—tu—tunataka kushirikiana na kusaidiana.

³⁵ Hili linaonekana ni jambo la kukufuru, lakini natumaini halionekani jinsi hiyo kwenu, Bw. Cory alisema wakati mmoja, yeye . . . Nilikuwa katika kampeni ya taa, nikiuza balbu za kampuni. Naye akanunua balbu nyingi sana ambazo zingemfaa kwa matumizi ya miaka minne au mitano, nikageuka na kununua Ford toka kwake. Yeye akasema, “Billy, ninaamini ni hali ya nipe nikupe.” Kwa hiyo huko ni, naam, kusaidiana tu kwa namna fulani katika wakati wa haja. Kwa hiyo hilo ni—hilo ni sawa. Tunajua jinsi ya kuokoana na kusaidiana.

³⁶ Sasa, hebu na tuiendee sehemu halisi ya jambo hilo sasa, na kama sikukosea, ninaamini ninamuona Ndugu Beeler kule myuma upande wa nyuma, ndugu mwingine mhudumu. Na leo nilipopitia hapo karibu, Ndugu Junie Jackson alikuwa amesimama nje hapa uwanjani pamoja na Ndugu Creech. Wanakuwa na ibada hapa wakati mwingine? Ibada ya ubatizo, sawa. Sawa, tunaweza kutoa maji kama watapata mtu wa kubatizwa. Sisi—sisi tuna maji, sawa.

³⁷ Kwa hiyo sasa, kwa vile tutakuwa na ushirika, nilifikiri ingekuwa vizuri iwapo ningezungumza juu ya ushirika kwa dakika chache tu.

³⁸ Sasa, kabla ya kulikaribia Neno, hebu na tuweke kando kila kitu sasa, na njia zetu zote za kijinga na za kitoto, na—na kuukaribia Uwepo wa Mungu kwa maombi. Hebu na tuombe. Sasa vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa, na naamini na mioyo yetu pia, kama kuna haja hapa ambayo inge . . . ungetaka ijulikane kwa Mungu, na ungetaka nikukumbuke mbele za Mungu, hebu ijulikane kwa kumwinulia Mungu mkono wako. Mungu na aijalie haja ya kila mtu.

³⁹ Mungu Mwenyezi, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye amemfufua Yeye katika wafu na kumketisha Yeye mkono wa kuume wa Ukuu, aishiye sikuzote kufanya upatanisho juu ya mambo ambayo tunaamini kwamba Yeye alitutendea sisi, na kukiri kwamba ndivyo ilivyo, tunaomba, Bwana Mungu, kwamba usiku wa leo, kwamba Wewe utatusamehe dhambi zetu. Loo, tunataka kukaa chini ya Damu wakati wote, kwani

hatujui ambalo lingetukia. Mambo yote karibu yamemalizika, tunahisi, Bwana, kwamba kuja kwa Bwana kumekaribia. Na tunajitayarisha kusafiri. Na tufikiriapo juu ya safari, twaweza tufikirie juu ya masanduku, na—na nguo za ziada na viatu vya ziada. Lakini jinsi hiyo ilivyo tofauti na safari hii! Si kufungasha, ni kufungua, kuweka kando. Kama mtumishi Wako mkuu, Paulo, alivyosema katika Kitabu cha Waebrania sura ya 12, “Tunaweka kando kila uzito na kutokuamini ambako hutuzinga kwa upesi, ili kwamba tuweze kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu.”

⁴⁰ Na hatuwezi sasa kutabiri mambo mazuri kwa ulimwengu huu wa kisasa. Jambo pekee ambalo tunaweza kutabiri kwa roho ni uharibifu, udhia, matetemeko ya ardhi, misukosuko mikuu ya bahari, jua na mwezi vikikoma, kanisa katika wakati wa Laodikia, Kristo nje ya mlango, akipiga hodi apate kuingia. Ee Mungu! Kama Mikaya wa kale, angewezaje kumbariki Ahabu wakati unabii ulikuwa dhidi yake? Wakati yule nabii mkuu mwenye nguvu, Eliya, alimwendea, na kwa sababu ameondoa uhai wa yule mtu asiyekuwa na hatia, Nabothi, kwa hiyo aksema, “Mbwa watairamba damu yako.” Basi Mikaya angewezaje kutabiri mambo mazuri?

⁴¹ Watoto wa siku hizi waliojazwa Roho watawezaje kuwatabiria mema wenye dhambi, watu wasiojali ambao wamemfungia Bwana nje? Ee Mungu, tunaona uchungu tu wa hukumu mbele yetu. Na kuwapigia makelele wale wasio sawa. “Mkimbileni Bwana kwani Yeye ni Mwamba katika nchi ya uchovu! Yeye ni mahali pa kujisitiri majira ya dhoruba. Na Jina la Bwana ni Ngome Imara, na wenye haki huikimbilia wakawa salama.” Twawezaje kufikiria juu ya ile miji mikuu iliyojengwa, ya makimbilio, na wakati mfukuzaji. . . anayemfukuza mtu naye akaingia katika ngo—ngome, alikuwa salama, hakuna kitu kingeweza kumgusa. Ee Mungu, tujalie tukimbie na tuharakishe kumwendea Bwana, kwani Yeye Ndiye Kimbilio letu na Nguvu yetu, na msaada wa karibu wakati wa mateso. Kwa hiyo, kwa kuona kwa jicho la tai, kama ilivyokuwa, matatizo yakitokea, mawingu yakizunguka, ngurumo na umeme wa hukumu vikiuvamia ulimwengu, tunajua kwamba tufani inakaribia.

⁴² Usiku wa leo, Bwana, tunawaombea hawa hapa ambao wameinua mikono yao. Sijui walitaka nini, Baba, Wewe unajua. Naomba kwamba utawapa kila kitu kwa ajili ya nafsi zao za thamani, ambao kwa makusudi hayo mkono huo umeinuliwa. Lijalie, Bwana. Waponye walio wagonjwa. Wafariji walio wachovu. Wape furaha wanaodhulumiwa. Wape amani walio wachovu, Chakula kwa wenye njaa, Maji kwa wenye kiu, furaha kwa wenye huzuni, uwezo kwa kanisa. Bwana, mlete Yesu miongoni mwetu usiku wa leo, tukiwa tunajitayarisha kushiriki ushirika unaowakilisha mwili Wake uliovunjwa-

vunjwa. Tunaomba, Bwana, kwamba Yeye atatuzuru kwa njia ya ajabu sana.

⁴³ Bariki kusanyiko hili dogo, mchungaji wake mpenzi, Ndugu yetu Neville na jamaa yake, na mashemasi, wadhamini, na kila mtu aliyepo. Wabariki wengine, Bwana, kila mahali ulimwenguni, ambao wanangojea kwa furaha kuja kwa Bwana, taa zimetengenezwa, na dohani zimesuguliwa kabisa, na Nuru ya Injili ikiangaza katika sehemu zenye giza.

⁴⁴ Sasa, nisaidie, Bwana, kwa maneno haya machache. Na libariki tunapolisoma Hilo, na utupe somo, kwa maana tunaomba jambo hilo katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁵ Sasa tunaweza kukifungua Kitabu, sura ya 6 ya Yohana Mt., na lingekuwa jambo jema kama kila mmoja wetu angesoma sura yote hii tuendapo nyumbani. Ningetaka kusoma, kuanzia aya ya 47, kuenda chini hadi ya 59, zote pamoja, kwa namna tu ya kujenga kifungu juu ya somo la ushirika. Yesu akizungumza sasa, kwenye sikukuu. Ulikuwa wakati mkuu, hizi sikukuu zilikuwa hivyo. Walikunywa maji toka mwambani, kuwakilisha ule Mwamba uliokuwa nyikani. Nao wakala, kwa ajili ya mana ile ambayo ilianguka miaka mia nyingi iliyopita, kwa ukumbusho. Ilikuwa tu ni sikukuu ya pasaka, kama tuliyo nayo usiku wa leo.

Amini, amini, nawaambia, Yeye aniaminiye Mimi yuna uzima wa milele.

Mimi ndimi chakula cha uzima.

Baba zenu waliila mana jangwani; wakafa.

Hiki ni chakula kishukacho kutoka mbinguni; kwamba mtu akile wala asife.

Mimi ndimi chakula chenye uzima kishukacho kutoka mbinguni; kwamba mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.

Basi Wayahudi walishindana wao kwa wao wakisema, Awezaje mtu huyu kutupa sisi mwili wake tuule?

Basi Yesu akawaambia, Amini, amini, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu.

Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.

Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli.

Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake.

Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi.

Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni; si kama mababa zenu walivyokula, wakafa, bali akilaye . . . chakula hicho ataishi milele.

Maneno hayo aliyasema katika sinagogi, alipokuwa akifundisha, huko Kapernaumu.

⁴⁶ Bwana na abariki neno Lake. Nataka tu, kwa dakika chache, kuzungumzia juu ya: *Ushirika*. Neno *ushirika* linamaanisha nini? *Kushiriki* humaanisha “kuzungumza.” Kuwa na *Ushirika* hasa kunamaanisha “kushirikiana, kuzungumziana.” Kama ukizungumza kwenye simu na mtu fulani, hapo mnazungumziana, mnashirikiana. Na kama tungenesoga kando na kusimama huko upande wa nyuma wa hili jengo, mtu ye yote na mchungaji, au watu wo wote wawili, wanashirikiana mmoja kwa mwingine.

⁴⁷ Sasa, hushirikiani kwa redio, kwa sababu hamwezi kujibizana, au televisheni. Lakini wakati unaweza kwa simu, kwa sababu mnashirikiana mmoja kwa mwingine, si upande mmoja. Ni . . . Siwezi kushirikiana nanyi sasa, kwa sababu hamjibizani nami. Kwa hiyo, basi, isingekuwa kuja kumsikiliza mchungaji akitoa ujumbe wake. Isingekuwa hivyo, kukusanyika pamoja, kushirikiana. Huo usingekuwa ushirika. Kama unakuja kushirikiana na mchungaji tu, ungelimwita kando, au mtu ye yote, na kushirikiana na huyo mwanamume au mwanamke.

⁴⁸ Lakini tunalolijia, ushirika, ni kwa kila mmoja wetu kama watu binafsi kushirikiana na Kristo. Huko ndiko kushirikiana. Basi, kushirikiana si kabisa mtu *mmoja* anayezungumza; sisi pekee kuzungumza, bali kungojea na kuona ambacho Yeye anatumia.

⁴⁹ Sasa hapo ndipo ambapo, mara nyingi, kwamba tunafanya makosa yetu makubwa, ni, tunaendelea kuzungumza na hatungojei na kumpa Yeye nafasi ya kujibu. Tunakwenda wakati mwingine, tunasema, “Bwana, ningemba kwamba Wewe utende *fulani na fulani na fulani na fulani*, amina,” na kuinuka na kuondoka. Sasa, huko kwa kweli sio kushirikiana. Huko ni kwenda na kuomba kibali. Lakini wakati unapokaa kirefu vya kutosha mpaka Yeye anajibu, hapo ndipo ambapo unapata ushirika, kushirikiana na Bwana. Naam, na njia kuu ya kushirikiana, ni kupatana, lazima mpatane juu ya mambo fulani. Sasa, na ni ajabu kwamba wakati mwingine tunapopata mambo hayo . . .

⁵⁰ Kula kunahusiana nalo. Sasa, wachukue wafanya biashara, wanapotaka kufanya mapatano ya biashara, watamwalika mtu kwenye chakula cha mchana. Na baada ya kuketi chini na kula, ndipo wanazungumziana. Mchuzi hodari, kwa kawaida

hawezi kuzungumza na mtu asiye na kitu tumboni. Ni bora zaidi kungojea mpaka yeye ajisikie vizuri, na basi baada ya kupata kiamshakinywa chake. Usiinuke pale na kumwamsha kitandani na kumwambia juu ya kitu ulichonacho cha kumuuzia, lakini ngojea mpaka amepata kiamshakinywa chake na—na amekaa sawa katika hali nzuri.

⁵¹ Hivi majuzi, nikihubiri juu ya yule mwanamke ambaye alimwosha Yesu miguu, huko Canada nilikuwa ninazungumza hili, nikisema kwamba wakati mgeni alipokuja kumzuru mtu mwingine, mtu huyu alikuwa na matendo fulani waliyopaswa kupitia kabla ya wao kujisikia wanaweza kuja kuzuru au kushirikiana. Kuzuru ni kushirikiana. Sasa, wangepikia kwenye...Kualikwa, kwanza ilikubidi ualikwe. Halafu ungefika mlangoni na mtumishi mwanamume angekuosha miguu, kwa sababu kusafiri, ulipatwa na harufu ya wa—ya wanyama na kadhalika barabarani. Wote...watu walisafiri barabara ile ile pamoja na wanyama, na—na halafu kulikuwa na harufu na vumbi, na mavazi ya Kipalestina yaliyaokota na yakakaa kwenye jasho la miguu, na sehemu ya uso ambayo haikufunikwa, na—na mikononi. Na—na wangewapokea mlangoni, mtumishi mwanamume angewapokea, akawaosha miguu. Kisha mtu mwingine alisimama pale na taulo na—na kibweta, nao wangenyunyiza hiki kibweta mikononi, nao wangepasugua hivi, na—na kuyapaka usoni mwao, halafu wakachukua taulo wakawapangusa. Hilo liliondoa uchafu wote na harufu. Nayo yangukuwa na kitu ndani yake ambacho kiliburudisha, kama menthol, na yaliwafanya wajisikie vizuri zaidi.

⁵² Basi walipoingia, sio na viatu vyako vikuu kuu na vichafu, hayo mazulia mazuri, wangukuwa na vitu vidogo kama sapatu za kuvalia nyumbani, nao wangepingia. Na halafu wa—wageni wangepingia ndani na—na halafu yule mwenyeji ange—angewapa busu la kuwakaribisha. Na, unaona, usingependa mwenyeji akubusu kama ulinuka vibaya. Usingependa kukanyaga mazulia huku u mchafu. Ndipo mwenyeji angekupa busu la kukukaribisha, na halafu ulikuwa mmojawapo wa nyumba ile.

⁵³ Na, sasa, Mungu ana mambo kama hayo. Kabla ya kuwa tayari kweli kwa kushirikiana na Mungu, lazima kwanza tuoshwe kwa maji ya Neno. Utenganisho, maji ya utenganisho ambayo hututenga na dhambi zetu. Sasa, jambo la kwanza, huwezi kuzungumza na Mungu na huwezi kushirikiana na Mungu, na kuna...Kwanza, yakubidi utubu yale uliyotenda, kwa sababu huwezi kuamini sawasawa mpaka unatubu, “Bwana, nisamehe kutokuamini kwangu.” Unaona? “Nisamehe kutokuamini kwangu.” Yakubidi utubu, kwanza. Na, unapotubu, basi wewe u...dhambi zako za nyuma zinasamehewa, basi u mmoja wa wanaobatizwa. Sasa, basi, Yeye aliahidi Roho Mtakatifu baada ya ubatizo.

⁵⁴ Sasa, jambo lenyewe ni hili, kwamba, katika ushirika huu, tunaona kwamba kulikuwa na—na kutawadhana miguu na mambo kama hayo, pia, kutawadhana miguu yetu, kama ishara ya kusafishwa na Roho Mtakatifu.

⁵⁵ Sasa, basi, lazima kuwe na upendano. Kama hauelewani na mwe—mwenyeji wako, basi ha—hamwezi kushirikiana. La, ha—hamwezi kufanya hivyo, kwa sababu hupatani naye. Lakini kama mnapatana, basi mnaweza kushirikiana. Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo tunapokuja kwenye meza ya Bwana, yatubidi tupatane na Neno Lake. Unaona? Yatubidi tuzaliwe mara ya pili, Roho wa Mungu ndani yetu akisema “amina” kwa kila Neno ambalo Yeye ameandika, ndipo tunaweza kushirikiana na Yeye.

⁵⁶ Hili tumeambiwa na Mungu, mioyo yetu isipotuhukumu, basi tuna kibali na Mungu. Tunajua tunapokea maombi yetu na dua yetu, ni kwa sababu mioyo yetu haituhukumu. Sasa, kama Mungu akituambia lazima tuzaliwe mara ya pili, na hatukupokea kuzaliwa upya, basi tutaona wasiwasi kidogo kumwendea, kumuomba Yeye kitu cho chote, unaona, kwa sababu tunajua hatujatimiza matakwa Yake. Kitu pekee basi ni sala ya mwenye dhambi. Lakini tunazungumza na Yeye tunaposhirikiana Naye, hilo huleta ushirika.

⁵⁷ Sasa, njia hii ya ushirika, ningetaka kuelezea kwa muda kidogo. Sasa, tunachukua, tunachoita *ushirika*, ni mkate na divai. Sasa, huo umeelezewa vibaya sana hata si vizuri kuuzungumzia. Loo, jinsi huo ulivyoelezewa vibaya kwenye miaka iliyopita! Huo kwa kweli sio ushirika, huko ni kushika amri. Unaona? Sasa, sababu ya sisi kuuita ushirika, ni kwa sababu linahusiana na neno la Kikatoliki ambalo ni “Ekaristi Takatifu, ambayo ni mwili halisi wa Bwana Yesu.” Lakini si mwili wa Bwana Yesu! Ni kumbukumbu tu la mwili Wake.

⁵⁸ Na sijali, makasisi wangapi au wahubiri, au ye yote anayeubariki huo, bado ni mkate na divai. Hakuna kasisi kama wanavyotuambia, kwamba, “Mungu anawajibika kumsikiliza kasisi wakati yeye anapogeza ushirika,” wanaoita ushirika, “Ekaristi, kuwa mwili halisi wa Bwana Yesu. Halafu mwamini anapokea huo, na huo ni ushirika.” Hayo ni makosa!

⁵⁹ *Kushiriki* ni “kuzungumza na, kushirikiana, kitu ambacho unaweza kukizungumzia nacho kitakujibu.” Huko ni kushirikiana. Mkate mwembamba hauwezi kujibu. Kwa hiyo, kwa kweli, ushirika wenyewe ni Roho Mtakatifu akijibu. Unapomwomba Yeye, basi Yeye anakujibu, huo ndio ushirika sahihi. *Hii* ni kumbukumbu, kushiriki katika kusulubishwa Kwake na kufufuka Kwake, na sio ushirika. Tunauita hivyo, lakini sivyo ulivyo. Ilitoka katika kanisa Katoliki, juu ya kushiriki mkate huu mwembamba kama tulivyozungumzia hivi majuzi katika utaratibu, na kulizungumzia katika *Ukristo Dhidi ya Ukafiri*.

⁶⁰ “Jinsi ambavyo mkate huu mdogo mwembamba ni mwili halisi wa Kristo.” Sasa, kanisa Katoliki huamini hivyo. Uliwahi kuona, wanapopita kanisani wanajifanyia alama ya msalaba, wanatoa kofia zao, na kadhalika. Si kanisa, ni ule mkate mdogo mwembamba mle ndani, “ule mwili ambao kasisi ameugeza kutoka mkate mdogo mwembamba ukawa mwili halisi wa Kristo,” na huku panya na vipanya wanaweza kuubeba. Mbona, huwezi, huwezi kuwazia mawazo ya kiungwana ukafikiria kwamba eti kipande cha mkate kingekuwa mwili wa Bwana Yesu! Haiwezekani.

⁶¹ *Ushirika* ni “kuzungumza, na kinajibu, kitu ambacho unazungumza nacho.” Neno lenyewe hasa *ushirika* humaanisha “kuzungumza na,” au, “kushirikiana na kitu ambacho kinakujibu.” Na Mungu hukuzungumzia pia, kushirikiana. Na bado ni mkate na divai, ambavyo tunaviita *ushirika*.

⁶² Sasa, Yesu alisema hapa, ninaposoma, “Mwili Wangu ni chakula na kinywaji, Damu Yangu, mwili na Damu ni chakula na kinywaji.”

⁶³ Sasa, tunataka kufikiria kumhusu Yesu na kumhusisha Yeye, kile alichokuwa Yeye. Mwili Wake ni nini? Mwili wa Kristo ni nini? Ni kundi la waamini ambao wanashirikiana na Yeye katika Roho Mtakatifu. Si sanamu, si kipande cha mkate, bali Roho ambaye yuko ndani ya moyo wa mwamini, nao wanashirikiana pamoja, kwamba wakati mwanadamu na Mungu wanaweza kuzungumza mmoja kwa mwingine, wana na binti za Mungu. Binadamu asiyedumu, kwa kumwaga Damu ilileta ondoleo la dhambi, na mtu huyu na mwanamke huyu, mvulana au msichana, ambaye ana ushirika pamoja na Kristo, anashirikiana Naye, mwili.

⁶⁴ Kama vile mume na mke wangeketi chini na kuzungumziana, au mvulana na mpenzi wake. Kriso na kanisa Lake wakishirikiana pamoja. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kusikia kutoka Kwake, na kuona wakati ujao kabla haujafika hapa, na kuweza kujua wakati ujao kwamba ni mkamilifu, kwa sababu tunashirikiana na yule Mungu anayeshikilia Umilele katika mkono Wake. Tukishirikiana mmoja kwa mwingine, mwili wa Kristo, mwili wa siri na wa kiroho wa Kristo. Si kuhusiana na aina yo yote ya sanamu, au mkate au d—divai, bali katika u—umbo la kiroho.

⁶⁵ Sasa, Yesu alisema jambo lile lile. Chukua Yohana Mt., sura ya 4, akizungumza na yule mwanamke pale kisimani. Yeye alikuwa akizungumzia kuhusu kitu kama, “Baba zetu walikunywa penye chemchemi hii, na wakachimba kisima hiki, Yakobo, naye—naye akawapa wanawe na wanyama wake, maji haya, Nawe unasema, ‘Tuabudie katika mji fulani,’ na wengine husema ‘Katika mlima huu.’”

⁶⁶ Kisha Yesu a—akasema, “Hebu kidogo! Sisi tu Wayahudi, nasi tunaelewa ni nini, maana ya kuabudu. Lakini sikiliza hili, ewe mwanamke. Saa inakuja, na sasa ipo, ambapo waabudu halisi watamwabudu Mungu katika Roho na katika kweli. ‘Neno Lako ni Kweli.’ Naye Baba huwatafuta watu kama hao wamwabudu Yeye katika Roho na katika Neno, ile Kweli. ‘Neno Lako ni Kweli.’ Sasa, Yeye alimwambia hayo yule mwanamke.

⁶⁷ Unaona, Kristo...Mungu ni Roho. *Kristo* humaanisha “mpakwa mafuta, mtu alipakwa mafuta na Mungu,” ambalo lilimfanya Yeye Kristo. Sasa, Kristo alisema, “Mimi ni Chakula na Kinywaji.” Si mkate mdogo mwembamba, si mkate mdogo mwembamba tunaokula hapa. Huo si Kristo. Divai tunayokunywa katika madhabahu sio Kristo. Inamwakilisha Yeye, katika mfano. Lakini Kristo ni Roho Mtakatifu, upako ambao uko juu ya Kanisa, hicho ndicho Chakula na Kinywaji.

⁶⁸ Kilio kikuu kuliko vilio vyote vilivyomo ulimwenguni mwote, natumaini hakuna mmoja wenu aliyewahi kukisikia, lakini, kama uliwahi kukisikia, hakuna kilio kinacholingana na kilio cha njaa. Unapomwona mama na mtoto wake mchanga, naye hawezi kutembea yu mnyonge sana, na mtoto yule machanga anakufa, na tumbo lake dogo limevimba kutokana na njaa, kusikia hivyo vilio vya kwikwi vikitoka kwenye moyo wa mama yule, unamwona mtoto huyo mwenye mashavu yaliyobonyea mpaka imebaki tu ngozi na mifupa, na mafizi yake madogo yanang’aa, naye hawezi kutoa sauti, ni vigumu kwake, macho yake madogo yametokeza. Hakuna kilio kama cha njaa na cha kiu.

⁶⁹ Huko nje jangwani, ni watu wangapi wamepoteza maisha yao kutokana na kiu! Hadithi nyingi, ambazo ningeweza kuwafanya mkae macho usiku kucha, kwa hadithi za kweli za jangwa. Jinsi ambavyo unapopata...unapopatwa na kiu, jinsi Shetani anavyokupa ma—mazigazi. Mmeyaona hapa, haikulazimu kwenda Magharibi kuyaona. Shuka uende barabarani, na inaonekana kana kwamba kuna maji barabarani. Kila mmoja wenu ameona jambo hilo, ambao mumeendesha magari na mnakuwa kwenye barabara kuu. Hayo ni mazigazi ya uongo. Hapa hivi majuzi, kama miaka mitatu au minne iliyopita, nilisoma ambapo baadhi ya bata, wakiruka kuvuka nchi, waliona mazigazi nao wakaanguka barabarani, wakifikiria walikuwa wameypata maji. Basi wakavunjika vipandevipande, walianguka barabarani kwa kishindo, wakifikiria walikuwa wanatua katika maji, mazigazi.

⁷⁰ Ni mara ngapi Shetani ametenda jambo lile lile kwa watu, akawapa mazigazi ya bandia, ambapo, hakuna kitu pale, lakini ni kiinimacho tu. Watu wengi sana leo hii wanapata dini ya kiinimacho, wakijaribu kutengeneza kitu au kujifanya kuna kitu wakati sivyo ilivyo! Kama maskini mwanamke yule mmishenari alivyosema kwamba alingojea mpaka akawa na

uhakika. Afadhali tufanye hivyo. Huwezi kurudi na kujaribu tena. Una nafasi moja, na una Ramani yake, kwa hiyo afadhali twende kwenye lengo letu.

⁷¹ Kilio cha njaa, sikiliza, ni kilio kikubwa kwa sababu ni kilio kilichojaa dhiki. Mtu huyo anakufa. Na, loo, laiti tungeliweza kufikia mahali pale, laiti taifa hili lingeweza kufikia mahali ambapo lina njaa ya Mungu sana! Liko katika hali mbaya ya kuwa na njaa sana kuliko mataifa kama ya India ambayo yanakufa kwa njaa kimwili, taifa hili linakufa kwa njaa ya kiroho. Lakini baada ya kuona njaa muda mrefu, inafikia mahali ambapo hujui una njaa.

⁷² Kama tu kuganda kwa baridi. Baada ya kufikia kiwango fulani, kuganda, unaona baridi sana, ndipo baada ya kitambo kidogo unapata joto. Na upatapo joto, unakufa! Na hiyo ndiyo shida usiku wa leo. Makanisa yamekuwa na baridi sana mpaka yanakufa kwa baridi, huku yakifikiri kwamba yana joto, kwa washiriki, nayo yanakufa kiroho. Kufa! Hayajui hivyo. Hatimaye, analala, ndipo amekwisha. Hainuki tena, kwa sababu damu yake imeganda katika mishipa yake.

⁷³ Sasa, kuona kiu. Yesu alisema, “Damu Yangu ni kinywaji cha kweli.” Kama unaona njaa kwa ajili ya uzima, unaona njaa kwa ajili ya uzima, Yesu ndiye tu aliye na maji yale yanayoweza kuzima kiu ile. “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo.” Katika Ufunuo, ilisema, “Yeye aliye na kiu na aje kwenye chemchemi ya maji ya Uzima na anywe bure.” Kama unaona kiu cha Uzima!

⁷⁴ Tunaona kwamba mamajusi wanabashiri, wakati fulani katika sehemu ya mwanzoni au sehemu ya kwanza ya mwezi, kuanzia kwenye tarehe mbili au tano, au wakati fulani mwezi huu, mamajusi wa Kihindi wanabashiri alimwengu utapasuka vipandevipande. Nayo magazeti ya Kimarekani yanadhihaki. Siamini dunia itapasuka vipandevipande, lakini ninasema ni makosa kulidhihaki. Kwa sababu, kitu fulani kiko karibu kutukia hivi karibuni, kitu kama hicho, wakati zile sayari tano, Mars, Jupiter, na Venus, na—na kadhalika, zijapo kwenye—kwenye...Hazijawahi kutenda hivyo. Loo, wanadai labda miaka ishirini na mitano elfu iliyopita, lakini ni nani alikuweko nyuma huko kujua jambo hilo?

⁷⁵ Ninabashiri kwamba hili lina matumizi ya kiroho. Ninaamini ni mwisho unaokuja wa hoja ya Mungu, kwamba mafunuo makuu ya Neno yatafunguliwa wakati huu. Kumbuka, wanadai ilikuwa nyota tatu zilizokuja kwenye mzingo wakati Yesu alipozaliwa. Na hii ni tano, na tano ni neema, namba ya neema. Tatu ni namba ya ukamilifu. Tano ni namba ya neema, J-e-s-u-s, n-e-e-m-a, i-m-a-n-i, na kadhalika. Namba ya neema! Mungu akiwahi kupeleka nguvu Yake kwa kanisa, itakuwa kwa neema Yake, haitakuwa ni kwa utii wa watu. Na Isaya

alisema, katika sura ya 40, jinsi ya “kuupazia sauti Yerusalemu, kwamba vita vyake vimekwisha,” hata hivyo ulikuwa na hatia ya ibada za sanamu, lakini ilikuwa neema ya Mungu iliyokuwa inakupeleka. Mungu anapotupelekea cho chote itakuwa neema Yake na si matendo yetu mema. Kwa hiyo, inaweza kumaanisha kitu fulani. Ninabashiri kwamba kutakuwa na badiliko. Sijui itakuwa ni nini, lakini ninaamini linajitayarisha kutukia. Tuko kwenye. . . katikati ya mkesho wake sasa.

⁷⁶ Na iwapo mtu ye yote anaona njaa, na aje kwa Kristo. Kama mtu ye yote ana kiu, na aje kwa Kristo. Yeye hutuliza kiu. Yeye ndiye Mridhishaji wa kiu yetu yote pamoja na njaa.

⁷⁷ Nilikuwa na hadithi ambayo nilihadithiwa wakati fulani uliopita. Pengine niliisimulia katika kanisa hili. Kama nimeisimulia, nisameheni kwa kuirudia ili nigusie sehemu iliyo muhimu. Kulikuwa na kiongozi wa Kihindi, au, namna fulani ya mwangalizi wa Wahindi. Alikuwa anatembea katika nchi ya Navajo, naye akapotea. Jina lake lilikuwa Coy. Naye alikuwa akitembea kwenye mkondo, mkondo wa wanyama pori, naye akawazia, “Sasa, kama nikiupata mburuzo huu, hakika nitapata maji.” Na farasi wake alikuwa na kiu sana mpaka ulimi wake ulikuwa unatokeza nje, mkavu, tundu za pua zilikuwa nyekundu na zimegandamana kwa mchanga. Alikuwa ameshikilia kitambaa chake usoni mwake katika pepo za vumbi mpaka ukagandamana, naye alikuwa anaangamia, kwa maji. Naye alikuwa anamwongoza farasi wake alipoupata ule mkondo. Naye akasema, alipopanda juu ya farasi aliona mkondo huu wa wanyama, akasema, “Hakika utanifikisha kwenye maji.” Kwa hiyo akashika hatamu za farasi wake na akaanza kushuka kwenye ule mkondo.

⁷⁸ Naye yule farasi alijua pia alikuwa kwenye mkondo unaoelekea kwenye maji. Jinsi Mungu anavyotoa silika kwa wanyama bubu! Basi akaenda moja kwa moja kwenye ule mkondo. Hatimaye, akapiga kona chache upande mmoja, chache tu sana kutoka kwenye ule mburuzo. Yule farasi alitaka kugeuka upande ule, lakini Coy alifikiria vinginevyo. Alijaribu kumshikilia katika ule mkondo wenyewe, naye akaanza kusonga mbele wala yule farasi hakutaka kwenda. Akamchokoa, naye akaliala na kuelekea upande mwingine. Ndipo akaanza kuinua miguu ya mbele. Alikuwa mnyonge sana asingeweza kumrusha chini.

⁷⁹ Kwa hiyo akaanza kuvuta vichokoo tena, mpaka akamkata yule farasi, akiwa ana shauku sana kuyafikia maji, maisha yake yangeokolewa, mpaka yule farasi akasimama, akitetemeka na kutokwa na damu. Basi akatazama chini, akatazama chini kule, alikuwa anatetemeka hivyo na karibu aanguke chini yake. Akainama akamwanguka, akaona damu ubavuni mwake. Alikuwa Mkristo. Naye akamwambia farasi wake, akasema, “Nimesikia mara nyingi kwamba wa mwituni. . .

au, wanyama wanayo silika. Haielekei kana kwamba kitu hicho kidogo kinachoelekea upande ule kingekuwa kinakwenda kwenye maji. Inaonekana kama njia hii kuu hapa ingeelekeza ambako wanakokwenda mara zote kunywa maji.” Lakini akasema, “Kama umenibeba kwa uaminifu hadi sasa, nitafuata silika yako.”

⁸⁰ Loo, jinsi ninavyofikiria hilo kumhusu Kristo! Njia iendayo kwenye uharibifu ni wazi na inaangaza kote, bali iko njia nyembamba iongozayo hadi Uzimani. Ni wachache wanaoiona. Yeye pekee, sio silika, lakini Roho Mtakatifu atakugeza akuelekeze kwenye maji hayo ya Uzima. Nafikiri, Huyo amenileta mimi salama umbali huu, nitamchukua Yeye njiani mwote.

⁸¹ Kumalizia ile hadithi, yeye—yeye hakwenda nusu maili, hadi, kwa ghafla, yule farasi mwaminifu alipojitumbukiza moja kwa moja kwenye shimo kubwa la maji. Yule farasi alijua ambalo alikuwa akizungumzia, alilokuwa anamaanisha katika njia yake ya kujieleza kwa yule—yule mpandaji. Yeye aliingia mle ndani. Alisema alitupia maji pua la yule farasi. Yeye mwenyewe akaoga, akalia kwa nguvu na akapiga mayowe, naye alikuwa akipaza sauti kwa nguvu zake zote, na kumwaga maji ndani ya koo lake, na kupaza sauti kwa nguvu, “Tumenusurika! Tumenusurika! Tumenusurika!” Naye yule farasi, akinywa, na kutetemeka. Naye akaangalia mbavu zake zenye damu, halafu zote zimejaa mikwaruzo ya vichokoo.

⁸² Na mara tu akasema, akasema...alimsikia mtu fulani akisema, “Toka humo majini.” Ndipo akaangalia, na palikuwa na maskini mchungu ng’ombe aliyeumbuka uso amesimama pale. Naye akatoka mle majini. Naye alisema alisikia harufu ya moto, ndipo akatazama upande wa juu, na kulikuwa na kundi la watu waliopiga kambi pale. Walikuwa kule na vyombo vya kuchunguza madini. Walikuwa wameigundua dhahabu, nao walipokuwa wanarudi walikuwa na farasi wao na farasi wa mizigo, basi wakaja kwenye kisima hiki cha maji nao walikuwa wanapumzika, na wote wamelewa.

⁸³ Naye akasema walikuwa wanapika mawindo, naye akala pamoja nao. Kisha kasema, mmoja wao akasema, “Kunywa pombe.” Akawaambia yeye alikuwa ni nani, yeye alikuwa ni Jack Coy, yule—yule kiongozi wa Kihindi. Kwa hiyo akasema, “Vema, sasa, kunywa pombe.”

Akasema, “La,” akasema, “Mimi sinywi.”

⁸⁴ Na hilo ni kama matusi kwa hao watu. Kwa hiyo akasema, “Tutakupa pombe unywe!”

Akasema, “La, sinywi.”

⁸⁵ Kwa hiyo akatupa lile kopo juu, akasema, “Kunywa pombe!” Wamelewa, wote, unajua, kama nusu dazani.

Na kwa hiyo akasema, “Asanteni, vijana.”

⁸⁶ Kasema, “Kama mawindo yetu ni mazuri vya kutosha kula, wiske yetu ni nzuri vya kutosha kunywa.”

⁸⁷ Na unajua jinsi walivyo, walevi. Naye akasema, “La,” akasema.

⁸⁸ Ndipo wakatia risasi katika bunduki, wakasema, “Sasa utakunywa la sivyo!”

⁸⁹ Kasema, “La. La, sitakunywa.” Naye akaanza kulenga raifoo. Kasema, “Hebu kidogo.” Akasema, “Mimi siogopi kufa.” Akasema, “Mimi—Mimi siogopi kufa.” Akasema, “Lakini mimi—mimi nataka kuwasimulia hadithi yangu kabla ya kufa, kwa nini mimi sinywi.” Kasema, “Mimi ni Mkentucky.” Akasema, “Na katika kibanda kidogo cha magogo asubuhi moja, ambapo mama alilala anakufa, aliniita kando ya kitanda chake, naye akasema, ‘Jack, baba yako alikufa ameshika jozi ya karata mkononi mwake, upande wa pili wa meza, amelewa.’ Akasema, ‘Usinywe pombe kamwe, Jack, hata ufanye nini.’” Kisha akasema, “Niliweka mikono yangu kwenye paji la uso wa mama yangu. Nami nikamwahidi Mungu, kama mvulana mdogo mwenye umri wa miaka kumi, nisingekunywa pombe yangu ya kwanza.” Akasema, “Sijainywa kamwe.” Ndipo akasema, “Sasa kama unataka kunipiga risasi, nipige tu.”

⁹⁰ Na wakati yule mlevi alipoinua bunduki yake na akatupa kopo juu tena, kasema, “Inywe au nitakupiga risasi.” Mara bunduki ikalia na lile kopo likapasuka.

⁹¹ Maskini mchungaji alikuwa amesimama kando ya genge huku ameumbuka uso, machozi yakimtiririka mashavuni mwake. Akasema, “Jack, mimi pia ninatoka Kentucky. Nilimwahidi mama siku moja, lakini nilivunja ahadi yangu.” Akasema, “Nilikuwa ninangojea mpaka jamaa hawa walewe vya kutosha, nami ningeliliva kundi lote, kwa vyo vyote, nichukue dhahabu yote waliyokuwa nayo.” Akasema, “Lakini nimekuwa mlevi na nimefanya kosa. Lakini,” kasema, “nina hakika wakati bunduki yangu ilipopiga mwangi kwenye magenge ya mbinguni, mamangu alinisikia nikiweka ahadi sitaifanya tena.” Na hapo, kwa neema ya Mungu, akawaongoza wote watu hao kwa Kristo, wote wale nje kule.

⁹² Unaona, kuna kitu fulani kuhusu maji, kitu fulani kuhusu kuburudika. Wazo langu lilikuwa, kufikia, kufika majini unapokuwa na kiu. Kuna kitu fulani yanachokutendea, ni kufika majini unapoona kiu.

⁹³ Sasa, Yeye alisema, “Amani yangu nawaachieni. Amani Yangu nawapeni.” Si kama ulimwengu uwapavyo amani, lakini jinsi Yeye awapavyo amani. Amani Yake hutuliza kiu yetu. Kama tunatamani amani, basi hebu na tuburudike katika amani Yake, kujua kwamba tuna amani na Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye Ndiye anayetupa amani ambayo hutuliza kiu yetu.

⁹⁴ Aya ile isemayo, “Yeye ni Chakula cha kweli na Kinywaji cha kweli.” Nina alama ndogo hapa, aya ya 57, “Chakula cha kweli na Kinywaji cha kweli.” Sikilizeni kile alichosema Yeye hapa.

Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi.

⁹⁵ Kwa maneno mengine, “Baba alinituma Mimi, Nami ni hai kwa Yeye. Na kila mtu ambaye huja kwa Kristo lazima aishi kwa Kristo.” Loo, jamani, hivyo ndivyo ilivyo, huo ndio ushirika. Huo ndio ushirika wa kweli unaopata wakati unapoishi kwa Kristo.

⁹⁶ Sasa, miili yetu huhitaji chakula na kinywaji kila siku, kuishi, miili yetu ya kawaida. Kama hatuli chakula kila siku na kunywa, basi miili yetu hudhoofika. Kuna kitu ndani yetu kwamba yatubidi tule chakula. Chakula cha siku moja hakitadumu kwa siku inayofuata. Yakubidi ule chakula kila siku, kuutia nguvu mwili wako unaokufa. Unaweza kuishi bila, lakini u mdhaifu zaidi. Na siku ya pili, bado u mnyonge zaidi. Na siku ya tatu, unakuwa mdhaifu kabisa.

⁹⁷ Vema, hicho ndicho ambacho mara nyingi tunatenda katika ulimwengu wa rohani. Unaona, kila siku yatubidi kushirikiana na Kristo. Yatubidi kuzungumza Naye kila siku. Yatubidi tupatane Naye kila siku. Paulo alisema, “Ninakufa kila siku.” Unaona? “Kila siku, ninakufa; hata hivyo ninaishi, si mimi bali Kristo huishi ndani yangu.” Kwa hiyo, kama mwili wako wa kawaida unahitaji chakula kila siku na maji kila siku, upate kuishi, mwili wako wa kiroho unahitaji Chakula cha kiroho na ushirika pamoja na Bwana kila siku, upate kuishi. Ndiyo. Yesu alisema, “Mtu hataishi kwa mkate tu, lakini kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.” Kwa hiyo, kila siku yatubidi kusoma Biblia. Watu wengine hawaisomi kamwe. Wengine huichukua kila mara mbili au tatu kwa mwaka. Lakini, mwamini wa kweli, wa kweli hasa, ambaye kweli amejengwa kiroho, huisoma Biblia yake kila siku, na kuzungumza na Bwana. Hiyo ni kweli. Yambidi kufanya hivyo. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.”

⁹⁸ Sasa, sababu nyingine ya sisi kula chakula, ni kujenga mwili wetu upate kuzuia maradhi. Kama huli chakula, na kuacha mwili wako udhoofike, basi ni rahisi kushambuliwa na magonjwa. Magonjwa yataambukiza mzunguko wako wa damu, ndipo yatakuangamiza. Kama damu yako si nzuri na safi, vema, basi itakuwa hivyo, magonjwa yataingia kwenye mzunguko wako wa damu. Kwa hiyo yakubidi ule chakula kizuri chenye nguvu kufanya mzunguko wako wa damu kuwa sawa. Kama huli, utadhuriwa na maradhi. Hiyo ndiyo shida kwa Wakristo wengi.

⁹⁹ Kama mimea ya kuotesywa kwenye nyumba ya kuoteshea. Unajua, ukiutoa mmea katika nyumba ya kuoteshea, yakubidi uubembezeze. Haujui hali ya hewa. Haujui mwanga wa jua na kadhalika, umefunikwa kila mahali na kubembeleza. Na hiyo ndiyo shida ya wengi sana wanaodhaniwa kuwa Wakristo, wao ni mimea inayootea nyumbani. Hiyo ni kweli, inashambuliwa na kila mdudu anayekuja hapo! Unajua, ndiyo pekee mi—mi—ndiyo pekee mimea dhaifu ambayo haina budi kupuliziwa dawa, au, mimea ya kuchanganyisha mbegu.

¹⁰⁰ Unajua ukimchukua mg'ombe mzee wa aina ya gredi na kumfungulia huko nje malishoni, na kumwachilia ng'ombe wa kienyeji nje kule, huyo wa kienyeji anaweza kufanikiwa kwa sababu ni mzao wa kiasili. Bali hebu mchukue wa kisasa au wa gredi ambaye amechanganyishwa mbegu, ni ng'ombe mzuri zaidi kwa kuonekana kwa macho, hakika, mnene zaidi na mwenye afya nzuri zaidi, lakini hebu waachilie huko na hawawezi kufanikiwa. Watakufa! Yawabidi washugulikiwe sana. Unaona?

¹⁰¹ Na hiyo ndiyo shida leo, tunao Wakristo waliovalia nadhifu zaidi, makanisa makubwa zaidi, na wingi wa—wa elimu, theolojia nyingi, lakini yabidi wabembeleze wakati wote, yakubidi utumie miwani yao ama sivyo huoni hata kidogo. Tunachohitaji ni Wakristo halisi, waliozaliwa chini ya Damu ya Bwana Yesu, ambao hawaishi kwa theolojia ya kanisa, lakini kwa Neno la Mungu, ushirika pamoja na Kristo. Neno likija katika mwamini, mwi—mwili wake wa kiroho unajengwa. Si mtoto wa nyumba ya kuoteshea!

¹⁰² Kulikuwa na mhudumu mmoja aliyesema leo, nilimsikia, alisema hivyo katika redio, alisema, kwamba alipokuja nchini, alikuwa na shida ya tundu ndani ya paji, nao walikuwa wakizungumzia juu ya kupasuliwa. Nao walisema kwamba watafanya *hivi* na *vile* na kumkata na kumpasua, na kuondoa sehemu ya kifuko cha paji, ambalo lingeubonyeza uso wake, na kadhalika, namna hiyo. Naye alisema amekula vidonge chungu zima. Ilielekea kwamba kulikuwa na vidonge vingi ambavyo ilimbidi atumie. Bali alipokuja kwa daktari mzuri wa Kikristo, yule daktari alisema, “Hebu na tusahau vile vidonge na hebu tusahau kule kupasuliwa na tuujenge mwili ili uweze kumpinga mwana sayansi.” Basi!

¹⁰³ Kuna nini kwamba watu hawaishi kirefu vya kutosha kama ilivyokuwa? Yatubidi tupate sindano kwa ajili ya *hilo* na sindano kwa ajili ya *lile*, na kujipulizia sisi wenyewe kila aina za madawa. Inafanya nini? Inatufanya tuwe debwedebwe, wanene, laini, tusiofaa. Ambapo watu wa kale... Mbona, tunadhuriwa na kila kitu. Sasa wanapata kudhurika zaidi na cho chote kile.

¹⁰⁴ Nimesimama Afrika, sikuweza kudungwa sindano ya Malaria. Lakini mbu wa Malaria angetua juu ya mkono wangu, ningepatwa na Malaria. Hawapigi kelele, na ni vigumu kwako

kujua. Wanatua, wanatua tu, basi umeisha yapata. Kama ukiishi, utakuwa nayo kwa miaka kumi na mitano. Na halafu wakati mwingine yanakuua. Na kulikuwa na wale wenyeji kwenye vibanda vyao vidogo huku mbu wamejaa miguuni mwao, nao ni uchi. Mbu Wametua juu yao, mbu wa malaria, nalo halikuwahangaisha. Kwa nini? Wamejijengea kinga. Walikuwa na chanjo waliyopewa na Mungu.

¹⁰⁵ Na hiyo ndiyo shida ya watu leo. Hiyo ndiyo shida kwa kanisa. Tuna sindano nyingi sana za kitoto, na theolojia iliyotengenezwa na mwanadamu, mpaka tumepuliziwa kila mahali. Tunachohitaji ni chanjo ya Mungu kwa Neno la Bwana Mungu. Mtu ataishi kila siku kwa Chakula cha aina hiyo, kujenga nafsi yake kutokana na maradhi ya kiroho ambayo yanasambaa na kuruka kila mahali nchini. Ninayo maandishi mengi juu ya jambo hili, lakini sina budi kukoma.

¹⁰⁶ Sasa, jijenge, jitayarishe kwa chanjo. Sasa, tunaishi kwa hii, miili—miili yetu lazima iwe na hii. Na, kama hatuishi kwa hii basi tunaweza kupata maradhi ya kila namna. Na Neno la Mungu, tunapoliamini na kulikubali kwa ushirika, “Bwana Neno Lako ni Kweli.”

¹⁰⁷ “Kanisa langu linasema haikulazimu kuzaliwa mara ya pili. Wanasema ‘kupeana mikono ni kuzaliwa mara ya pili.’ Wanasema ‘kunyunyiziwa maji.’ Wanasema mambo haya mengine yote ‘Ni kweli, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.’” Lakini Biblia ilisema kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Unaona? Sasa, wewe endelea na sindano hizo za kubuniwa na watu ukitaka, utajifanya mwenyewe Mkristo wa uongo. Unaona? Hutaki jambo hilo.

¹⁰⁸ Huwezi kupata Uhai isipokuwa tu kupitia kwa Kristo. Na sasa Neno Lake linafanya nini? Linaujenga mwili wetu wa kiroho, imara, tunaposhirikiana na Yeye, kumpinga Shetani.

¹⁰⁹ Wewe unasema, “Ndugu Branham, ni nini hicho unachosema, ‘kushirikiana katika Neno Lake?’”

¹¹⁰ Ndiyo, Yeye ni Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Nasi yatupasa kuula mwili Wake. Basi mwili Wake ni Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Neno. Naye alisema, katika Yohana Mt. 15, “Ninyi mkikaa ndani Yangu, na ushirika Wangu, Neno Langu, likikaa ndani yenu, basi mwaweza kuomba mtakalo nanyi mtatendewa.” Basi. Hiyo ni kweli. Unaona, ombeni mtakalo!

¹¹¹ Unafanya nini? Unaujenga mwili wako upate chanjo kutokana na . . . Mtu fulani anaingia akasema, “Loo, kanisa letu haliadini katika kupaza sauti.” Unaona, umejengwa. Nini? Una ushirika ndani yako, Neno. Na umechanjwa kwa huo. Kama upuzi mtupu ukija, ni nini? Hauna Neno ndani yake, basi wewe una hakika ni kosa. Sijali linaonekana halisi jinsi gani, kama si

Neno liache. Kweli, liache. Sijali linafanya nini, lazima lilingane na Neno!

¹¹² Katika maombi, kama nilivyokuwa ninamnukuu Mikaya akisimama pale, angalia, ulionekana sawa hasa, wakati Israeli iko hapa, na sehemu hiyo ya nchi ilikuwa ni mali yao. Wale wageni wameingia na kuichukua kutoka kwao na wamejenga nyumba zao wenyewe, nao walikuwa wanakulia sehemu ya nchi ambayo Mungu aliwapa. Kwa hiyo ilionekana kama wale manabii mia nne wa Kiebrania walikuwa sahihi. Lakini, unajua, kulikuwa na kitu fulani kumhusu Yehoshafati kilichokuwa cha kiroho, alisema, “Je, huna mwingine?”

¹¹³ Akasema, “Ninaye mwingine, lakini,” kasema, “ninamchukia. Jambo pekee analofanya ni kutabiri uovu.”

Kasema, “Nenda ukamwite tukamsikize.”

¹¹⁴ Naye akakwea, akasema, “Endeleeni, kweeni huko, lakini nimemwona Israeli ametawanyika kama kondoo wasiokuwa na mchungaji.” Ndio akasimulia ona lake.

¹¹⁵ Sasa, ni wa nani sahihi? Ilionekana kama wale mia nne walikuwa sahihi. Watu mia nne waliofunzwa vizuri, wakisema, “Kwea, Bwana yu pamoja nawe,” Na hata Zedekia alikuwa—na—na—alikuwa... Zedekia alikuwa ametengeneza pembe mbili kubwa za chuma. Akasema, “Kwa hizi utawasukuma wale wageni kutoka nchini.” Alikuwa na hakika yeye alikuwa sahihi. Yeye alijua alikuwa sahihi. Lakini, unaona, alikosea.

¹¹⁶ Huyu hapa Mikaya, mmoja dhidi ya mia nne, naye alisema, “Kama ukikwea, Israeli atatawanyika, bila mchungaji,”

¹¹⁷ Na hao wengine wakasema, “Kwea, Bwana yu pamoja nawe!” Sasa, kimali, walikuwa sahihi, sehemu ile ilikuwa mali ya Israeli. Lakini Neno la Mungu lilikuwa limemhukumu Ahabu, kwa hiyo Mungu angeweza kubariki ambacho Yeye amelaani?

¹¹⁸ Ndivyo ilivyo hapo leo hii... Unaona? Neno la ushirika lilikuwa ndani ya Mikaya. Sasa, kama unashirikiana na Mungu katika kuzungumzia ushirika halisi, na roho aliye ndani yako hapatani na Neno hili, hushirikiani na Mungu, unashirikiana na mashetani. Na wanaigiza sana! Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho karibu wangewapoteza walio Wateule kama yamkini. Bali mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita.” Na kama Paulo alivyosema, Wagalatia 1:8, “Kama malaika kutoka mbinguni akihubiri Injili nyingine yo yote isipokuwa hii mliyokwisha kusikia, na alaaniwe.” Hata malaika! Katika kanisa la mwanzoni, wakati watu wale, kama Mtakatifu Martini, Ireneo, hao watu wacha Mungu, wakati Shetani angejitokeza kama malaika wa nuru. Lakini, wewe angalia, atakuwa kidogo nje ya Neno.

¹¹⁹ Alimtokea Hawa kama malaika wa nuru, akamwambia, “Hakika, Bwana alinena *hili*, Bwana alinena *hili*,” lakini

mwishowe kabisa hakukubaliana na Mungu. Na hivyo ndivyo ushirika wa uongo ufanyavyo leo. Wakati watu wanapofikiri wanamwomba Mungu, nao hawatalitii Neno, ni ushirika wa uongo.

¹²⁰ “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo,” unaona, “na mtatendewa.” Sasa, haliwezi kufanya kazi wakati mmoja, halafu lishindwe wakati mwingine. “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakikaa ndani yenu,” yaani, yadumu mle. *Kukaa* humaanisha “kubakia hapo, kudumu papo hapo.” Ndiyo, hilo—ni kuchanjwa dhidi ya maradhi ya dhambi.

¹²¹ Sasa, hebu nifunge kwa kusema neno hili moja sasa, kabla ya kufika kwenye meza ya ushirika. Damu na Mwili wa Bwana, vikichanganyikana na imani, hiyo ni Damu na Mwili, hilo ni Roho na Neno, vikichanganywa na imani, ni sawasawa na Uzima wa Milele. “Aulaye Mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa Milele, Nami nitamfufua siku ya mwisho.” Basi. Ni nini? Ushirika wa Bwana. Neno na Roho, Uhai huu uko katika Damu, Neno na Roho ni sawasawa na Uzima wa Milele, kwa imani katika Bwana.

¹²² Hili hapa ombi langu, ninapooni mwisho unakaribia na kuona, dakika yo yote, kitu fulani kingeweza kutukia, na kujua kwamba hatuko mbali na Kuja kwa Bwana. Bwana, basi katika Jina la Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, hebu nichukue Neno, ule Upanga, na kuuinua Huo kwa imani niliyo nayo, na kufyeka nipate njia katika kila nguvu ya pepo, mpaka nimwone Yesu, kwa kushiriki Neno Lake.

¹²³ Kushirikiana na Neno Lake. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani Yenu, basi niombeni Mimi mtakalo nanyi mtatendewa.” Jinsi inavyopendeza! Huo ndio ushirika halisi na Neno na Roho, na imani ya kuutumia Huo, “Ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa.” Hebu na tuombe.

¹²⁴ Baba Mtakatifu na Mwenye Rehema na Mkuu, Mungu, yule MIMI NIKO mkuu, yule El Shaddai, kwa Ibrahimu. Ee Mungu, jinsi ambavyo ushirika huu mkuu wa Bwana ulivyo sawa na Uzima wa Milele, na jinsi ambavyo Huo unavyochanja dhidi ya majivuno, jinsi Huo unavyochanja dhidi ya kutokuamini, jinsi Huo unavyochanja dhidi ya dhambi ya ulimwengu. Ni ushirika, pamoja na upendo wa Kiungu kwa Baba yetu wa Mbinguni. Na kwa haki ya Yesu Kristo tunaikaribia meza hii. Nasi twaomba, Bwana, kwamba Wewe utatupa kila mmoja wetu kukaribia huko usiku wa leo, katika Roho. Tusamehe. Nasi tunataka miili yetu ya kiroho ikue. Hatujali kuhusu kujiunga na kanisa fulani au madhehebu. Tunataka kujenga mwili wa kiroho, kwa kuchanjwa kwa dhambi, hadi kufikia mahali ambapo hakuna tena hamu ya kutenda mabaya, na ambapo Roho Mtakatifu anaweza kuchukua Neno Lake Mwenyewe miongoni mwetu na

kulinena vipya kama lilivyonenwa siku ile, kwa sababu ni Roho yule yule ambaye alikuwa katika Bwana Yesu. Ninaomba, Baba, kwamba utatupa hilo.

¹²⁵ Wakati unamalizika. Kwamba ni lini, hatujui, ambapo yule wa mwisho ataokolewa. Bali ninaomba usiku wa leo, Bwana, kama kuna hao hapa ambao hawakujui Wewe kama Mwokozi wao, hebu wakuone wewe usiku wa leo wanapokuja kwenye maji haya ya ubatizo, kama kumbukumbu, kuungama kwa mwili huu wa waamini ambao wanaamini habari kwamba Yesu wa Nazareti alizaliwa na bikira Mariamu, akauwawa, akasulubiwa na Pontio Pilato, kisha akafufuliwa siku ya tatu na Mungu, na anaketi mkono wa kuume wa Ukuu, usiku wa leo, akiishi kutuombea.

¹²⁶ Lijalie, Bwana, kwamba mtu yule yule, akitii amri za Biblia, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu. Kwani hakuna jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu likupasalo wewe kuokolewa kwalo.” Ee Mungu, watu na waone ukweli wake, na Neno lililo thabiti. “Hakuna jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu likupasalo wewe kuokolewa kwalo isipokuwa katika Jina Lake Yesu Kristo.” Kwa hiyo, mtume alisema “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa kila wakati, kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Jalia, Bwana, kwamba kutakuwa na kuita kwingi usiku wa leo.

¹²⁷ Na imenenwa pia, na Bwana wetu, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Mgeni, na kama mgeni akizungumza, sauti ambayo si ya kimaandiko, upesi kondoo wataitambua. Ee Mungu! Na iwapo ni Sauti Yako, Biblia, yale isemayo, kila kondoo ataisikia Hiyo, kwa sababu Hicho ndicho Chakula cha kondoo. Wameshiriki. Wanajua Baba hulisha Chakula cha aina gani. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.” Jalia, Bwana, kwamba wengi wataona na wataelewa, na watakuja Kwako usiku wa leo.

¹²⁸ Wale wasio na Roho Mtakatifu, jalia wasiahirishe saa nyingine. Yaweza imechelewa sana katika saa nyingine. Wanaweza wasiwepo hapa.

¹²⁹ Na, Baba, kwa vile tulivyokusanyika sasa mezani kushiriki huu unaowakilisha mwili Wako uliovunjwawunjwa, tunaomba kwamba kama kuna dhambi katikati yetu, Bwana, tusamehe. Wewe ulisema, “Mkusanyikapo, mngoJane.” Mungu, kama kuna dhambi katika kusanyiko hili, mahali po pote, naomba kwamba Damu ya Yesu Kristo itamtenganisha mtu yule na dhambi yake, au mwanamke yule, mvulana au msichana. Pia, Baba,

ninajiombea mimi mwenyewe, kwamba Wewe utanitenga na kila shaka, kila dhambi, kila kutokuamini, cho chote kile. Tunajua kwamba kutokuamini ni dhambi. Ndiyo dhambi pekee iliyopo. “Yeye ambaye haamini amekwisha kuhukumiwa.” Na dhambi pekee iliyopo, ni kutokuamini Neno la Mungu. Na, Baba, kama kuna kutokuamini ndani yangu, nisamehe, Ee Mungu, nako ni kwingi, nami naomba kwamba Wewe unisamehe mimi. Samehe kusanyiko langu ambalo Wewe umenipa usiku wa leo, na uwalishe kwa Neno. Tujalie.

¹³⁰ Na tunaposhiriki kumbukumbu hizi ndogo za mwili uliovunjwa wa Yeye Ambaye amefufuka katika wafu na yu hai sikuzote miongoni mwetu, tujalie tuupokee ushirika toka Kwake, Bwana, ushirika wa Roho Mtakatifu. Tukirimie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹³¹ Sasa, kwenu ninyi ambao mnapaswa kwenda na hamwezi kukaa kwa zile dakika kama kumi na tano za ibada ya ushirika. . . Hatumo wengi, nasi tutashiriki ushirika. Si ushirika wa faragha. Bila shaka ni kwa kila Mkristo mwamini. Mungu hana mstari uliochorwa kati ya Mbatisti na Mmethodisti, na kadhalika. Sote, kwa Roho mmoja, tumebatizwa katika Mwili mmoja, nasi tu wenyeji pamoja wa Ufalme wa Mungu. Na kama kuna mtu fulani miongoni mwetu ambaye ni mgeni, mimi sipo hapa mara nyingi, na sijui ni yupi aliye mshiriki na yupi siye. Kumbuka, haidhuru u wa kanisa lipi, hilo si kitu. Kuna Kanisa moja tu, kwa vyo vyote, na hujiungi nalo, unazaliwa ndani yake. Hiyo ni kweli. Nawe unazaliwa katika Kanisa hili la Mungu. Nasi twaomba kwamba utampokea Kristo usiku wa leo, kushiriki Naye tunapokumbuka mwili Wake uliovunjwa na vitu hivi vidogo tunavyoshiriki, vya pasaka, na Mungu anyunyize mioyo yetu na dhamira zetu kwa Damu.

¹³² Basi wataleta ushirika, na tutasoma sasa toka 1 Wakorintho, sura ya 12. Na tutafanya ushirika mara baada ya jambo hili, nasi tunaamini kwamba Mungu atawabariki sana. Basi mara tutakaposoma au kabla hatujalisoma, kama inakubidi kuondoka, vema, unaweza kutoka uende kwa urahisi. Na halafu uwe pamoja nasi Jumatano usiku, na Jumapili asubuhi na Jumapili usiku. Kama unaweza kubaki kufanya ushirika pamoja nasi, tutafurahia sana ukifanya hivyo. Halafu mara baadaye, itakuwa ya Bwana. . . itakuwa ibada ya ubatizo, ambayo itakuweko katika dakika kumi na tano, au ishirini ikizidi sana, nafikiri. 1 Wakorintho, sura ya 11, aya ya 23.

. . . mimi nilipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku. . . aliotolewa alitwaa mkate,

Naye akiisha kushukuru akaumega, . . . kasema, Utwaeni, mkaule: huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.

Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, ninyi mnaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.

Basi kila ambaye hataula huo...kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.

Maana alaye na kunywa, isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.

Kwa sababu hiyo wako wengi kweni walio hawawezi na ni wadhaifu, na...kadha wa kadha wamelala.

Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isiye ikatupasa hukumu pamoja na dunia.

Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, ngojaneni ninyi kwa ninyi.

¹³³ Sasa, hebu muda kidogo wa sala ya kimya kwa kila mmoja wetu, niombeeni wakati ninapowaombea. [Ndugu Branham anatulia kidogo—Mh.] Kirimia maombi haya, Mwenyezi Mungu. Tusamehe makosa yetu kama sisi nasi tuwasameheavyo wale waliotukosea. Haya tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹³⁴ Hivi vifurushi vidogo ambavyo ni mkate wa kosha uliotengenezwa bila mafuta, kukolezwa, kadhalika, ambao unawakilisha mwili wa Bwana. Si wa duara, umevunjwavunjwa katika vipande vyote. Ni kwa sababu unamaanisha mwili Wake uliovunjwavunjwa ambao ulivunjwavunjwa kwa ajili yetu. Mungu na ajalie baraka Zake kwa kila mtu aulaye. Sasa, si ule mwili, unawakilisha tu mwili. Sina uwezo, wala hakuna mwingine aliye nao, kuufanya cho chote ila mkate. Mungu pekee. Na hivyo ndivyo Yeye alivyotuambia, kuula mkate huu na kukinywea kikombe hiki cha divai. Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

¹³⁵ Mungu Mtakatifu mno, ambaye sisi tu watumishi Wake, katika Jina la Yesu Kristo, takasa mkate huu kwa madhumini uliokusudiwa, kutufanya sisi, tunapoupokea, kukumbuka kwamba Bwana wetu alisulubiwa: na mwili Wake, uliokuwa wa thamani na mtakatifu, ulichanganywa na mapigo na miiba

na misumari, kwa ajili yetu, kwamba kupitia mwili Wake uliipasuliwa kulitoka Roho anayetupa Uzima wa Milele. Tujalie, Bwana, tunapoula, tupate neema ya kusafiria, kama Israeli alivyotenda miaka arobaini nyikani, pasipo hata na mtu mmoja mnyonge miongoni mwao. Baba Mungu, jalia jambo hili, tunapokuomba Wewe utakase mkate huu, makate wa kosha, kwa matumizi uliokudiwa. Katika Jina la Yesu. Amina.

¹³⁶ Kikombe cha Agano Jipya, Damu. Ninafikiria wimbo ule, “Tangu nilipoona kwa imani kijito kile kibubujikacho toka kwenye jeraha Zako, upendo wa ukombozi umekuwa ndio jambo langu kuu, na utakuwa hivyo mpaka nife.” Nionapo damu hii, zabibu, damu ya zabibu, ninajua inawakilisha Damu ambayo ilitoka kwenye mwili wa Bwana Yesu. Jalia kila apokeaye hii awe na Uzima wa Milele, magonjwa na yatoweke kwenye miili yao, uchovu na unyonge, kukandamizwa, jalia Ibilisi (katika kila hali) awaache, ili waweze kuwa na nguvu na afaya na Uzima wa Milele, kuacha nuru yao iangaze mbele ya kizazi hiki kibaya na cha zinaa tuishimo, kumtukuza Mungu.

¹³⁷ Baba wa Mbinguni, tunakuletea Wewe uzao wa mzabibu. Katika Jina la Yesu Kristo, utakase, kuwakilisha Damu ya Mwanao, Yesu, katika Hiyo tunapata, “Alichubuliwa kwa maovu yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Jalia, Bwana, kwamba Uhai ule utakuja kwetu, Uzima wa Milele kwa wingi, ili tupate kukutumikia vyema zaidi, tuwe na nguvu na afya kutuchukua toka mahali hadi mahali ambako tunatarajia kukutumikia Wewe, po pote utakapotuita. Jalia baraka hizi katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.



USHIRIKA SWA62-0204
(Communion)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marriion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Februari 4, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org